# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA







## ZIARA ZA KAMATI ZA KUDUMU ROBO YA NNE MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Tarehe:11 - 16, Agosti 2022

Katika robo ya nne ya mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo huanza mwezi Machi hadi Juni Kamati za Kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela zimefanya ziara ya kukagua miradi mbalimbali kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo ikiwa ni pamoja na kutoa maelekezo mbalimbali ili kuweza kutatua changamoto zinazojitokeza.

Kamati hizo za Kudumu ni Kamati ya UKIMWI, Kamati ya Huduma za Uchumi, Afya na Elimu, Kamati ya Mipangomiji, Ujenzi na Mazingira, Kamati ya Fedha na Uongozi.




*Ilemela ni yetu, Tushirikiane kuijenga*
*Imeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*

## YALIYOMO

Ukurasa wa 1
Ziara ya kamati ya ukimwi



Ukurasa wa 2
Ziara ya kamati ya Huduma za Uchumi, Afya na Elimu



Ukurasa wa 3
Ziara ya kamati ya Mipangomiji, Ujenzi na Mazingira



Ukurasa wa 4
Ziara ya kamati ya Fedha na Uongozi





11 Agosti, 2022

# ZIARA YA KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI











## Habari kwa Ufupi

Kamati ya Kudhibiti UKIMWI katika robo ya nne ya Mwaka wa fedha 2021/2022 imetembelea na kuangalia shughuli za kuhudumia WAVIU katika vituo vya kutolea huduma za tiba na matunzo (CTC) ambavyo ni Kituo cha Afya Sangabuye, Zahanati ya Igogwe na Zahanati ya Kiloleli Chamwenda.

Wakiwa katika vituo hivyo waliweza kupata taarifa kuhusiana na wateja waliopima VVU, idadi ya wateja ambao wapo kwenye huduma ya dawa pamoja na changamoto mbalimbali zinazokabili vituo hivyo

Baadhi ya changamoto zilizobainishwa ni pamoja na mahudhurio hafifu ya wateja kutokana na kazi zao za uvuvi za kuhama hama, mazingira yasiyo rafiki (hayana usiri) ya kutolea huduma za UKIMWI wateja kujihamisha bila kutoa taarifa, upungufu mkubwa wa Watumishi

Wajumbe wa kamati walihitimisha kwa kuwapongeza watumishi wa afya kwa kazi kubwa wanayofanya huku wakisisitiza kuendelea kutolewa kwa elimu kwa wateja wanaohama kutoa ripoti ili waweze kuendelea kupata dawa kule wanakohamia.

*Ilemela ni yetu, Tushirikiane kuijenga*
*Imeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*



14 Agosti, 2022

# ZIARA YA KAMATI YA HUDUMA ZA UCHUMI,AFYA NA ELIMU











TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

*Ilemela ni yetu, Tushirikiane kuijenga*
*Imeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*

## Habari kwa Ufupi

Kamati ya huduma za uchumi,elimu na afya ya Manispaa ya Ilemela katika robo ya nne 2021/2022 imefanya ziara ya kutembelea na kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo ya Afya iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa yenye thamani ya jumla ya kiasi cha shilingi 153,800,000 ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

Wajumbe wa kamati hiyo wamepongeza kwa ukamilishaji wa wodi za mama na mtoto katika zahanati ya Nyakato na zahanati ya Ilemela ambazo tayari zimeanza kutumika.

“Hakika tunaona unafuu na urahisi unaopatikana katika utoaji huduma kwa kina mama na watoto wao sambamba na maboresho ya mazingira ya kazi kwa watumishi wa maeneo husika.”Mhe. Andrew Nginila Mwenyekiti wa Kamati

Ilemela kupitia mapato yake ya ndani imeendelea kuboresha miundombinu ya huduma za kijamii ili kuhakikisha jamii ya inapata huduma bora na sahihii

Akihitimisha Mwenyekiti alisisitiza kuwa ziara ijayo Kamati itembelee vituo vya kutolea huduma za afya vya binafsi



15 Agosti, 2022

# ZIARA YA KAMATI YA MIPANGOMIJI, UJENZI NA MAZINGIRA











## Habari kwa Ufupi

Katika robo ya nne ya mwaka wa fedha Kamati ya Mipangomiji, ujenzi na Mazingira ilipata fursa ya kutembelea na kufuatilia Mradi wa upimaji Viwanja wa Nyafula, Mradi wa Viwanja wa Masemele, na Mradi wa Jengo la Makao Makuu ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.

Lengo la ziara hii ilikuwa ni kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo ili iweze kuleta tija pamoja na kushauri juu ya masuala mbalimbali.

Kuhusu mradi wa upimaji viwanja wa Nyafula, wajumbe walielekeza fidia iliyobaki kiasi cha Tsh. 1,300,000,000.00 ilipwe haraka ili viwanja viweze kuuzwa na suala la upimaji wa viwanja liwe endelevu kwani Ilemela bado inayo maeneo ya kutosha.

Kwa upande wa suala la ulipaji wa fidia zitokanazo na Ardhi, wajumbe walikubaliana kuanza kulipwa kwa fidia hizo kwa kuangalia ni madai yapi yalianza

Wajumbe walihitimisha kwa kuwapongeza wataalam kwa utekelezaji wa miradi inayoendelea huku wakisisitiza kufanyia kazi maelekezo yote yaliyotolewa na kamati.

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

*Ilemela ni yetu, Tushirikiane kuijenga*
*Imeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*



16 Agosti, 2022

# ZIARA YA KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI











## Habari kwa Ufupi

Kamati ya Fedha na Uongozi ni kamati ambayo inahusika na masuala yote ya kuidhinisha fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Katika robo ya nne ya mwaka wa fedha 2021/2022 imetembelea na kukagua miradi ambayo inatekelezwa na iliyokamilika kwa lengo la kuhakiki thamani ya fedha na utekelezaji wa miradi kama unaendana

Miradi waliyotembelea ilikuwa ni Hospitali ya Wilaya, Stendi mpya ya Mabasi ya Nyamhongolo, shule ya Sekondari Buzuruga, Shule ya Msingi Kangaye pamoja na nyumba ya mwalimu wa Shule ya Msingi Buswelu aliyeunguliwa na moto.

Wajumbe wa kamati hii walipongeza kwa namna miradi ya maendeleo inavyotekelezwa huku wakishauri masuala mbalimbali ikiwemo:

Kuhakikisha majengo ya hospitali ya wilaya yanakamilishwa, katika stendi ya Nyamhongolo waligusia suala la changamoto ya wafanyabiashara wanaovamia eneo la stendi litatuliwe kwa haraka na kuhakikisha stendi inatunzwa ili iweze kudumu kwa muda mrefu Katika shule ya Buzuruga walishauri ujengwe uzio kuzunguka shule.

Ziara ilihitimishwa kwa kumtembelea mwalimu aliyeunguliwa nyumba na kushauri apewe Shilingi Milioni nne ili iweze kumsaidia kukarabati nyumba hiyo.

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

*Ilemela ni yetu, Tushirikiane kuijenga*
*Imeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*